**ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu. |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/ /Jimbo la Ziwani. |

| | |
|---|---|
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |
| 13.Mhe. Juma Duni Haji | MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais. |
| 14.Mhe. Zainab Omar Mohammed | MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais. |
| 15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan | MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni. |
| 16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna | MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge. |
| 17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya | MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais. |
| 18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui | MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni. |
| 19.Mhe. Said Ali Mbarouk | MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando. |
| 20.Mhe. Haroun Ali Suleiman | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi. |
| 21.Mhe. Haji Faki Shaali | MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni. |
| 22.Mhe. Machano Othman Said | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni. |

| | |
|---|---|
| 23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan | MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole. |
| 24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu) | Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka. |
| 25. Mhe. Zahra Ali Hamad | Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake. |
| 26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo | Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki |
| 27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake. |
| 28.Mhe. Haji Mwadini Makame | Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi. |
| 29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi | Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni. |
| 30.Mhe. Mohammed Said Mohammed | Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae. |
| 31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak | Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake. |
| 32.Mhe. Said Hassan Said | Mwanasheria Mkuu. |
| 33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Jimbo la Chonga |
| 34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali | Jimbo la Mkoani |
| 35.Mhe. Abdi Mosi Kombo | Jimbo la Matemwe |
| 36.Mhe. Ali Mzee Ali | Kuteuliwa na Rais |

| | |
|---|---|
| 37.Mhe. Ali Salum Haji | Jimbo la Kwahani |
| 38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Nafasi za Wanawake |
| 39.Mhe. Asaa Othman Hamad | Jimbo la Wete |
| 40.Mhe. Asha Abdu Haji | Nafasi za Wanawake |
| 41.Mhe. Asha Bakari Makame | Nafasi za Wanawake |
| 42.Mhe. Ashura Sharif Ali | Nafasi za Wanawake |
| 43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 44.Mhe. Farida Amour Mohammed | Nafasi za Wanawake |
| 45.Mhe. Fatma Mbarouk Said | Jimbo la Amani |
| 46.Mhe. Hamad Masoud Hamad | Jimbo la Ole |
| 47.Mhe. Hamza Hassan Juma | Jimbo la Kwamtipura |
| 48.Mhe. Hassan Hamad Omar | Jimbo la Kojani |
| 49.Mhe. Hija Hassan Hija | Jimbo la Kiwani |
| 50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Jimbo la Bububu |
| 51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu | Jimbo la Mji Mkongwe |
| 52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub | Jimbo la Muyuni |
| 53.Mhe. Kazija Khamis Kona | Nafasi za Wanawake |
| 54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk | Jimbo la Kitope |
| 55.Mhe. Marina Joel Thomas | Kuteuliwa na Rais |
| 56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) | Jimbo la Mkwajuni |
| 57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma | Jimbo la Bumbwini |
| 58.Mhe. Mohammed Haji Khalid | Jimbo la Mtambile |
| 59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali | Jimbo la Uzini |

| | |
|---|---|
| 60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi | Jimbo la Chambani |
| 61.Mhe. Mussa Ali Hassan | Jimbo la Koani |
| 62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | Nafasi za Wanawake |
| 63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi | Nafasi za Wanawake |
| 64.Mhe. Nassor Salim Ali | Jimbo la Rahaleo |
| 65.Mhe. Omar Ali Shehe | Jimbo la Chake-Chake |
| 66.Mhe. Panya Ali Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 67.Mhe. Rufai Said Rufai | Jimbo la Tumbe |
| 68.Mhe. Raya Suleiman Hamad | Nafasi za Wanawake |
| 69.Mhe. Saleh Nassor Juma | Jimbo la Wawi |
| 70.Mhe. Salim Abdalla Hamad | Jimbo la Mtambwe |
| 71.Mhe. Salma Mohammed Ali | Nafasi za Wanawake |
| 72.Mhe. Salma Mussa Bilali | Nafasi za Wanawake |
| 73.Mhe. Salmin Awadh Salmin | Jimbo la Magomeni |
| 74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | Nafasi za Wanawake |
| 75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | Jimbo la Mwanakwerekwe |
| 76.Mhe. Subeit Khamis Faki | Jimbo la Micheweni |
| 77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Jimbo la Konde |
| 78.Mhe. Suleiman Othman Nyanga | Jimbo la Jang'ombe |
| 79.Mhe. Ussi Jecha Simai | Jimbo la Chaani |
| 80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla | Nafasi za Wanawake |
| 81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Nafasi za Wanawake |

**Ndugu Yahya Khamis Hamad** **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

**Kikao cha Tano - Tarehe 28 Oktoba, 2014**

*(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)*

**DUA**

*Mhe. Mwenyekiti, (Mahmoud Muhammed Mussa) alisoma Dua*

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuwasilisha Mezani Hati ya Mswada naomba kutoa taarifa ya kuwasilisha mbele yako na mbele ya Baraza la Wawakilishi, Tangazo Namba 93 la Mwaka 2014 kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Shahada ya Kuwasilisha Miswada ya dharura chini ya kifungu cha 80 cha Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Mhe. Rais ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi naomba kusoma hati ifuatayo:-

Kwa uwezo niliopewa chini ya kifungu cha 80 cha Kanuni ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar za Mwaka 2012.

Mimi Dokta Ali Muhammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Natamka kwamba Mswada wa Serikali wa Sheria ya Serikali za Mitaa na Mswada wa Serikali wa Sheria za Tawala za Mikoa ni ya dharura na ya haraka sana na kwamba haiwezekani kutimiza masharti ya kanuni ya 79.

Imetiwa saini na muhuri wa Rais tarehe 27 mwaka 2014. Naomba kuwasilisha.

Baada ya kuwasilisha Hati ya Dharura sasa naomba kuwasilisha Mezani Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Baraza la Manispaa Nam. 3 ya Mwaka 1995 na Sheria ya Halmashauri za Wilaya na Mabaraza ya Miji Nam. 4 ya Mwaka 1995 na Kuanzisha Upya Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa za Zanzibar ya Mwaka 2014 kwa Madhumuni ya Kuanzisha Serikali za Mitaa, Uwezo wake Kazi na Wajibu, Muundo, Mpangilio, Fedha na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha.

**Mhe. Mwenyekiti:** Asante Mhe. Waziri, sasa kabla hatujamkaribisha Mwenyekiti, tutamwita tena Mhe. Waziri. Mwenyekiti wa Kamati tunakuomba.

**Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria:** Asante Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 32(1), naomba kuwasilisha Hati Mezani ya Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Kuanzisha Upya Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2014. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

## MASWALI

### Nam. 45

### Hatari ya Kambi za Jeshi Kuwa Karibu na Makaazi ya Raia

**Mhe. Saleh Nassor Juma (Jimbo la Wawi) - Aliuliza:-**

Kwa kuwa maeneo ya kambi za Majeshi yetu humiliki silaha mbali mbali za hatari ambazo nyengine wachilia mbali kutumiwa, siyo vyema hata kuonekana na raia wa kawaida. Na kwa kuwa kambi zetu nyingi zipo karibu na makaazi ya raia kama vile kambi ya TPDF ya ALI KHAMIS CAMP iliyopo Vitongoji na hata ile iliyopo Ngerengere katika Jimbo hilo hilo la Wawi. Na kwa kuwa nchi yetu imeshashuhudia madhara kadhaa kwa raia wa kawaida yaliyosababishwa na kuripuka kwa vifaa vya kijeshi kwa upande wa Tanzania bara.

Je, ni lini Serikali itafikiria kuzihamisha kambi zetu za kijeshi zilizopo karibu na makaazi ya raia na kuzipeleka nje ya miji na vijiji.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais - Alijibu:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 45 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili na wananchi kwa jumla tukaelewa kwamba, katika nchi yoyote ile duniani kambi za kijeshi huwekwa kimkakati (*strategically*) kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalma katika nchi. Kwa msingi huo huo kambi za kijeshi zote zilizopo nchini zimewekwa kwa kuzingatia haja ya kiulinzi na usalama na mazingira ya nchi yetu na vilevile uwekaji wa miundo mbinu ya mawasiliano. Aidha, majeshi yetu yanahitaji maeneo maalum ya kufanyia mazoezi ili kujiweka tayari kwa uvamizi wa adui wan chi yetu wakati wowote. Lengo kuu la kuundwa kwa

majeshi yetu ni kuweka ulinzi na usaama na haya yote yanafanyika kwa ajili ya kuwalinda wananchi na mali zao na sio kwa ajili ya mbwebwe.

Mhe. Spika, hata hivyo, napenda pia ieleweke kwamba kambi zilizopo hivi sasa ni kambi ambazo zilijengwa kwa miaka mingi iliyopita na kwa wakati huo maeneo hayo hayakuwa karibu na makaazi ya raia. Tunachoona sasa ni matokeo ya baadhi ya wananchi wetu katika vipindi tofauti kuhamishia makaazi yao katika maeneo ya karibu na makambi ya kijeshi. Hili ni tatizo ambalo sisi viongozi na wananchi tunahitaji kulifanyia kazi ili kuona maeneo yetu tuliyoyatenda kwa ajili ya majeshi yetu yanahifadhiwa na kuheshimika. Serikali itaendelea na juhudi za kuelimisha wananchi waachane na tabia ya kujenga karibu na maeneo ya kasmbi za kijeshi ili kuepuka usumbufu na madhara yanayoweza kutokea. Hivyo serikali haina mpango ya kuhamisha makambi hayo katika maeneo yaliopo.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri katika Ofisi ya Makamo wetu wa Pili wa Rais, Mhe. Muhammed Aboud Muhammed naomba nimuulize suali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa dhamira kubwa ya kuanzisha jeshi letu ni kulinda mipaka pamoja na raia wetu. Na kwa kuwa wewe mwenyewe umekiri kwamba kuna ongezeko la watu na makambi haya yalipojengwa ilikuwa watu bado hawajaongezeka. Na kwa kuwa umekiri kwamba lazima wapate sehemu ya majeshi kufanya mazoezi. Na kwa kuwa katika Kambi yetu ya Ali Khamis Camp iliyopo Vitongoji pamoja na hii Ngerengere Wawi hapa wanafanya mazoezi wapiganaji wetu katika eneo la *County Side* ya Kisiwa cha Pemba, Makaani kule karibu na bahari ya Hindi na mizinga yote inaelekezwa kwenye bahari ya Hindi huko na sio huku uraiani.

a) Je, haoni kwamba ni busara kubwa, vile vyombo vya kufanyia mazoezi amana zao zikajengwa kule, ili kuepusha maafa kama yaliyotokea Mbagala huku ukitilia maanani kwamba silaha tunazotumia nyingi ni za zamani.

b) Kwa kuwa mambo ya kijeshi ni siri na hatutakiwi raia kuyafahamu kienyeji tu hivi; ni utaratibu gani mliochukua serikali wa dharura ili kuzihakiki hizi silaha zilizopitwa na wakati katika kambi zetu hizi zilizopo hapa visiwani Zanzibar, ili zisije zikafyatuka na kuanza kuzua zogo kama lililozuka kule Mbagala na kuhatarisha maisha ya watu.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, ni kweli anachosema kwamba katika kambi yetu ya Jeshi iliyopo Vitongoji na pale Wawi, mazoezi ya askari wetu mara nyingi wanayafanya katika eneo la kule Magharibi ambalo ni eneo kwa muda mrefu limetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Lakini ikumbukwe pia kwamba kabla ya wananchi kuhamia katika eneo lile la kambi zetu mbili za pale Vitongoji ilikuwa maeneo yale hayakukaliwa na wananchi wengi hapo awali. Na ni kweli sasa baada ya kukua kwa miji wananchi wamesogea karibu na makambi yale.

Mhe. Mwenyekiti, lakini uwamuzi wa kuwa na Makambi yale kama nilivyosema mwanzo ni ya kimkakati ya kiulinzi. Maeneo yale yamewekwa makusudi kwa sababu ni eneo maalum la kulinda nchi yetu. Ndio maana silaha na mambo mengine ya kijeshi yanawekwa katika maeneo yale, kwa madhumuni hayo. Na kwa sababu tu kwamba hakuna eneo la karibu ambalo litakuwa jeupe kwa kufanyia mazoezi ndio maana wanakwenda katika maeneo mengine kufanya mazoezi licha ya kufanya mazoezi pale.

Mhe. Mwenyekiti, lakini eneo lililofanyika mazoezi kimkakati wa kiulinzi sio vyema kupeleka Kambi yetu kuweko kule na bado umuhimu kambi iliyokuwepo pale ndio maana imebaki kuwepo pale. Kwa hiyo ndio maana ushauri mkubwa tunaotaka kufanya ili kunusuru maisha ya wananchi wetu ni kwamba wasiendelee kujenga karibu na makambi yetu ya jeshi, wakae mbali na makambi yetu ya jeshi ili tuwape nafasi wanajeshi wetu watulinde vizuri kwa maslahi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli yaliyotokea kule Dar-es-Salaam yanaweza kutokea mahali popote katika nchi yetu. Lakini uhakiki unaendelea kufanywa. Nataka nimuhakikishie Mhe. Saleh, kwamba Kambi zetu za hapa Zanzibar na Tanzania kwa jumla zipo salama.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Asante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa suali alilouliza Mheshimiwa Maalim Saleh Mwakilishi wa Wawi linafanana na ninalotaka kuuliza la Wananchi wa Unguja Ukuu. Pale hapana Kambi na hapana gharama yoyote kuondosha eneo kuwatafutia eneo jengine.

Mhe. Naibu Spika, ukizingatia jeshi kwanza anakuwa raia ndio anakuwa jeshi. Eneo lile tayari limeshaanza kuuwa si mara ya kwanza, si mara ya pili si mara ya tatu. Hii mara ya mwisho watu waliokota chuma wakakichukua kwenda kukifua ili watengeneze nanga ya ngalawa baadaye kikaripuka na mtu mmoja akafariki. Hapana gharama yoyote, serikali haioni kutafutia eneo jengine ili wananchi wa Unguja Ukuu ambapo wenye eneo lao kwa muda

mrefu ili wapate kutumia kwa shughuli zao za kilimo. Ukizingatia jeshi ni raia. Je, yupi ni muhimu kati ya jeshi na raia.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, popote katika nchi yetu sasa utapokwenda wapo raia, kwa hiyo ni kuondoa tatizo sehemu moja ukalipeleka tatizo sehemu ya pili. Jambo ambalo la msingi ni kushauri kwamba wananchi wasisogelee maeneo haya. Hapo lilipotatizo tubaki kuwepo nalo. Cha msingi jeshi letu linachukua kila hatua kuhakikisha tahadhari zinafanywa ili yasitokee madhara.

Mimi napenda sana nilipongeze jeshi letu hasa kwa upande wa Zanzibar. Tumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba hakuna tatizo kubwa lililotokea tokea kuwepo kwa makambi haya. Ushauri wangu bado naendelea kusema kwa wananchi wenzangu kwamba tuepuke sana kujenga karibu ya makambi na tukilize sana ushauri unatolewa na majeshi yetu katika kuchukua hadhari ya mambo mbali mbali ambayo yanaweza kuleta hasara kwetu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Kuhusu utaratibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Suali langu nimeuliza ni lini watatafutiwa eneo askari wale, pale hapana kambi na huenda wakitumia eneo lile kwa shabaha tu.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Waziri majibu ya nyongeza.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais:**Mhe. Mwenyekiti, naomba nijibu tena majibu ya nyongeza kwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ninalotaka kusema Mheshimiwa utakwenda kuwapeleka wapi? Ukiliondoa tatizo hapo ambapo Mhe. Jaku Hashim Ayoub anasema, yeye Mhe. Jaku anashauri tuwapeleke wapi ambapo hapana watu. Maeneo yote yamekaliwa, utakapowaweka popote pale itaathiri sehemu hiyo. Askari wetu wamefanya pale kwa sababu zao maalum za kiuaskari. Mimi sio mtaalamu wa askari na Mhe. Jaku, nadhani na yeye sio mtaalamu. Sisi haja yetu tuwe salama, tunawaweka askari wetu watulinde, nchi yetu iwe salama na ndio maana tunakuwa salama.

Mhe. Mwenyekiti, nataka tulipongeze sana jeshi letu hili kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya. Sasa tusiwabugudhi bugudhi wao wanafanya mambo kwa maslahi yetu sote na wanafanya mambo kwa kupima sana. Hawana nia ya kuwaathiri wananchi wetu, nia yao ni kutulinda. Inapotokea bahati mbaya inakuwa ni bahati mbaya, lakini dhamira ni njema. Mheshimiwa pale ndio

maamuzi kwa sasa yalipoamuliwa na jeshi letu waendelee kuwepo na watakuwepo. Kwa sababu utakapokwenda popote pale, pengine unalichukua tatizo sehemu moja unalipeleka sehemu nyengine.

**Nam. 23**

**Zanzibar na Ahadi ya Uwanachama wa Fifa**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Jimbo la Muyuni) – Aliuliza :-**

Uongozi mpya wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) baada ya kuchaguliwa walifika Zanzibar na kutoa ahadi kuwa watahakikisha Zanzibar inapata uanachama wa Shirikisho la Kabumbu Duniani (FIFA) chini ya mfumo wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ni muda mrefu sasa umepita hakuna hatua zilizofikiwa hadi sasa kuteleza ahadi hiyo.

(a) Kwakuwa ahadi kama hizo zimekuwa za kawaida kutolewa na viongozi wa TFF Serikali imechukuwa hatua gani za kuondoa tabia kama hiyo ya wananchi wake kudanganywa na viongozi wa vyama vya mpira wa miguu.

(b) Kitendo cha kutoa ahadi hiyo kinatoa sura gani kwa nchi wakati FIFA yenyewe ilishatoa msimamo kuwa Zanzibar haiwezi kupata uanachama katika mfumo wa Muungano uliopo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo –** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suali lake Nambari 23 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo mwaka 2012 nimewahi kujibu suali hili la Zanzibar kujiunga na FIFA kwa kutamka wazi ndani ya Baraza lako hili tukufu kwamba Shirikisho la Soka Duniani (FIFA) limetoa msimamo kuwa Zanzibar haiwezi kuwa mwanachama wa FIFA.

**Mhe. Mwenyekiti: (anaendelea)** Mhe. Naibu Waziri anajibu maswali ambayo yalikuwa yameulizwa nanyi, sasa tukiendelea kuongea kama hivi itakuwa hamumsikii nini anachokizungumza. Naomba tumsikilize ili tufikie malengo tuliyojiwekea. Mhe. Naibu Waziri tuendelee.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo –** Alijibu :-

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo mwaka 2012 imewahi kujibu swali hili la Zanizbar kujiunga na FIFA kwa kutamka wazi ndani ya Baraza lako tukufu kwamba Shirikisho la Soka Duniani (FIFA), limetoa msimamo kuwa Zanzibar haiwezi kuwa mwanachama wa Shirikisho hilo kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ni mwanachama wa FIFA ndio inayojulika kuwa ni Taifa na Chama cha soka cha Tanzania (TFF) ndicho kinachowakilisha Taifa hilo. Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa ufafanuzi huo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo haina taarifa kwamba uongozi mpya Chama cha Soka cha Tanzania (TFF) kimeahidi kuipatia Zanzibar uanachama wa FIFA.

b) Ikiwa kweli imetolewa ahadi hiyo sisi tunaomba dua iwe hivyo, lakini kwa ukweli itakuwa ni ahadi iliyokuwa haiwezi kutekelezeka kwani FIFA imeshatoa msimamo wake juu ya suala hilo.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali inatambua kabisa mpango wa kupata wanachama FIFA ni mgumu je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kuwa ZFA inaingiza angalau wajumbe wawili katika chombo cha TFF ili kuleta sura nzuri ya Muungano. Hilo la kwanza.

Kwa FIFA kila mwaka inatoa ruzuku karibu miaka 3 je, Zanzibar imenufaika katika mgao huo kiasi gani na nini kilichofanyika.

**Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mwakilishi nimeeleza kuwa Zanzibar haiwezi kuwa mwanachama wa FIFA na Mhe. Mwakilishi ninakushangaa sana kwa sababu wewe ulikuwa upo kwenye Bunge la Katiba na maelezo yaliyotolewa kwa kina na ufafanuzi mkubwa uliotolewa, nakushangaa leo hii ukiwa ni Mjumbe wa Bunge la Katiba ukaweza kuuliza swali ambalo limetolewa ufafanuzi wa kutosha kwenye Bunge la Katiba, na mwaka 2012 liliulizwa swali hili japo kuwa si mwakilishi wewe lakini mwakilishi mwengine aliuliza na Mhe. Waziri akasema tunajiandaa kwenda kwenye Bunge la Katiba, tuweze kuwa na mikakati kulizungumzia swali hili.

**Utaratibu**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Nilichouliza mimi ni Kiswahili wala si kihindi wala si kilugha ajibu kama nilichomuuliza kama yeye ni Naibu Waziri na Mhe. Rais kasisitiza nijibu. Kama huna jawabu Mhe. Naibu Waziri sema nitakujibu kwa maandishi maswali mawili niliyokuuliza. Jibu kama nilivyokueleza kama hujafahamu nambie nilichokizungumza. Mambo ya Bunge la Katiba yameshapita. Hujasikia nikuulize tena nilivyokuuliza, huna uwezo niambie nitakujibu kwa maandishi. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Mjumbe zungumza na kiti sio unazungumza na anayejibu maswali.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante, nilichomuuliza kwa kuwa Serikali inajua kabisa mpango wa kujiunga na FIFA ni mgumu je, kuna utaratibu gani wa kuingiza angalau wajumbe wawili katika chombo cha TFF ili kuleta sura nzuri ya Muungano.

La pili kuna mgao uliotolewa na FIFA karibu miaka 5 Zanzibar imenufaika na mgao huo, kitu gani kilichofanyika Zanzibar.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti na baada ya majibu mauzuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuongezea majibu ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza swali lake la mwanzo kuhusu kupata wajumbe wawili kwenye TFF ushauri wake tunaupokea tuweze kuufanyia kazi ili tuhakikishe kwamba tuwe na wajumbe zaidi ya hawa ambao Mhe. Jaku anawazungumza ili tuweze kuwakilishwa vizuri na TFF kwa kuwa ni chombo cha Muungano, ambacho kinapaswa kiwe na ushiriki wa kutosha na Zanzibar. Kwa hivyo ushauri wako ni mzuri na tunaupokea.

Kuhusu mgao; mgao tunapata na zinatumika fedha hizi kwa mafunzo kwa vijana wetu katika michezo mbali mbali. Kwa hivyo tutazidi tu kusimamia vizuri zaidi ili mgao upatikane mwingi hata hivyo baadhi ya matengenezo ya viwanja pia tunayatumia kwa mgao huo tunaoupata kutoka kwa wenzetu wa TFF. Ni jambo zuri kukaa na wenzetu tukajua kwa kina hasa kikajulikana kiwango sahihi ambacho Zanzibar ingepata. Tutashauriana na Wizara husika ili ushauri huo tuufanyie kazi vizuri. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri sana na ya kushangaza ya mawaziri wawili naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo lenye vifungu (a) na (b).

Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu ameonesha wazi kwamba Wizara yake inaomba dua ili tufanikiwe kupata wajumbe angalau wawili kwenye TFF. Je, sasa dua ile ambayo inayombwa itakuwa ni ya Wizara tu au nchi nzima ili tujuwe siku gani ya kuomba dua.

Lakini (b) Mhe. Waziri wa Nchi anasema kwamba kuna mgao ambao Zanzibar unapata kupitia TFF anaweza kutwambia ni shilingi ngapi kwa mwaka uliopita Zanzibar imepata.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza kuhusu mgao tunaoupata ambao unatokana na utaratibu wa TFF kutokana FIFA kiasi ambacho nilikipata mwaka jana kwa sababu ni suala la takwimu siwezi kulieleza hapa, lakini nitampa jibu hilo kwa maandishi ili tulipate kwa ufanisi na wajumbe wote watapewa taarifa hizo. Kwa hivyo naomba Mhe. Hija apokee hilo. Lakini nataka nimuhakikishie tu kwamba mgao huu ambao tunapata umesaidia sana katika matengenezo ya viwanja vyetu mbali mbali hapa Zanzibar kwa maana ya Unguja na Pemba. Kwa hivyo ni utaratibu mzuri uliopo.

Isipokuwa napenda tu nilihakikishie Baraza lako Tukufu kwamba tutawasiliana na Wizara husika tuone mambo haya yanafanyika vizuri na yeye mwenyewe anajua namna gani Uwanja wa Gombani ulivyofanyiwa matengenezo kupitia mgao huu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuweza kupata nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili swali la nyongeza. Pamoja na majibu yake mazuri sana Mhe. Waziri, Mhe. Waziri ametueleza kuwa hana data za uhakika za kuweza kujibu maswali aliyoulizwa na mjumbe. Je, Mhe. Waziri kwa kuwa hili suala ni muda mwingi sana tena ni mrefu, huoni Mheshimiwa kusema hivyo mbele ya Baraza hili kuwa huna data hizo inaonesha kuwa Wizara yako iko dhaifu sana katika kufatilia masuala haya.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, kutokuwa na data ni jambo la kawaida la ubinaadamu na hili swali la nyongeza si swali ambalo limepangwa kwamba mimi kichwa changu kitaweza kujua mambo yote kwa wakati mmoja. Lakini ni utaratibu wetu wa kibunge hapa kwa mambo yanayohusu Takwimu kuzipata takwimu za uhakika na ujibu kwa uhakika, hii matokeo yake ni kuheshimu Baraza lako Tukufu na hufanyi mambo kwa kupayuka payuka kama anavyotaka Mheshimiwa Mwakilishi. Kwa hivyo napenda nimhakikishie kwamba tunafanya mambo haya kwa umakini mkubwa na kwa kuheshimu Baraza ili majibu ya uhakika na sahihi.

**Nam. 65**

**Vifaa vya Uokozi kwenye Vyombo vya Kienyeji vya Usafiri**

*(Mjumbe aliyeuliza swali hili ameliondoa)*

**Nam. 76**

**Matrekta ya Wizara ya Kilimo**

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub –** Aliuliza :-

Hivi karibuni Wizara ya Kilimo imepata matrekta kumi (10) kwa upande wa Pemba na kumi (10) kwa upande wa Unguja. Hata hivyo kuna taarifa ya kusikitisha kuwa matreka manne (4) kati ya hayo yamechukuliwa na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ.

(a) Ni sababu gani Wizara ya Kilimo ikanyanganywa matrekta hayo.

(b) Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ haina bajeti kwa kuweza kuagiza matrekta yake.

(c) Je, huoni kuchukua matrekta hayo ni kuzorotesha shughuli za kilimo ambapo zingefanywa kupitia matrekta hayo yaliyochukuliwa.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili –** Alijibu :-

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Maliasili naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni swali lake nambari 76 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo na Maliasili haikunyang'anywa matrekta yake kama alivyouliza Mhe. Mwakilishi bali ni utaratibu wa kawaida wa kimajukumu na kiutendaji uliotumika na Vikosi vya SMZ wakiwa ni miongoni mwa wadau wetu muhimu wa kilimo hivyo tuliona upo umuhimu na haja ya kuwaptia matrekta hayo nao waendeleze kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na suala la Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum kuwa na bejeti ama kutokua nayo, Wizara ya Kilimo na Maliasili ikiwa ni miongoni mwa taasisi za SMZ kama zilivyo taasisi nyengine ilipokea agizo kutoka Ofisi ya Rais Ikulu na baada ya kupokea agizo hilo tuliamua kulitekeleza kwa kuzingatia kwamba hizi zote ni

taasisi zenye azma na dhamira moja ya kuleta maendeleo na mafanikio kwa wananchi wake. Sisi sote ni watoto wa baba na mama mmoja hatuna haja ya kubaguana.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na suala ama hoja ya Mhe. Mwakilishi kipengele (c) ni kwamba kuchukua matrekta hayo hakuwezi kuzorotesha kilimo kwani kazi ambayo ililengwa kufanywa na kutumia matrekta hayo na Wizara ya Kilimo na Maliasili ndio kazi hiyo hiyo ambayo itafanywa na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum kuwalimia wananchi pamoja na kulima katika mashamba yao ya Vikosi kwa azma ile ile tuliyoitaja hapo juu.

**Mhe. Jaku Hashim Ayoub:** Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu yaliyokuwa hayana afya ya Mhe. Naibu Waziri na ya kusikitisha yeye mwenyewe shahidi, Mwenyezi Mungu anatuona katika Kamati alikuwepo Mbweni kuhusu suala hili, mimi nilivyofanya kwa niaba ya Kamati, Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo. Leo amechukua hatua gani ya kuelimisha kwa Wizara ya Vikosi vya SMZ na Wizara ya Kilimo kuwa ndugu baba mmoja, mama mmoja kuelimisha wananchi ili kupata kufahamu. Lengo langu sio baya ni kuisaidia Wizara ya Kilimo baada ya kuona upungufu wa matrekta.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Mhe. Mwenyekiti, Mhe. mwakilishi suala la kuelimisha Wizara zote mbili kama sisi ni ndugu baba mmoja, mama mmoja nadhani sote tunajua hakuna asiyejua kwa sababu sisi sote tuko katika Serikali moja, Serikali ndio baba yetu, Serikali ndio mama yetu. Kwa hivyo ikiwa Serikali ndio baba yetu na Serikali ndio mama yetu mimi sioni vibaya kwamba kupeana kitu ambacho kilichotoka katika Serikali moja ile ile.

**Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:** Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Katika majibu yake alieleza kwamba matrekta yale ameyatoa Wizara ya Kilimo ameyapeleka Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa kule na Vikosi Maalum au Idara Maalum. Mimi nilitaka kujua tu kwamba kwa sababu hizi Wizara kila Wizara ina bajeti yake. Je, matrekta yale wamewagaia, wale Tawala za Mikoa wamewaazima, au wamefanyaje? Vile vile nilikuwa nataka kujua ni utaratibu upi waliotumika, wamehaulisha kupeleka kule au vipi. Maana Wizara ni mbili tofauti na kila moja ina bajeti yake. Ahsante.

**Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, Mheshimiwa matrekta hatukuwagaia, sisi tumeingia katika mkataba mkubwa na SUMA JKT baada ya kupata amri kutoka Ikulu kwamba tuwape matrekta yale tulifanya mkataba mdogo baina ya Wizara ya Kilimo na Wizara husika.

Ina maana baada ya kufanya huo mkataba mdogo tayari sisi na Wizara husika tunalipana. Wanatupa hivi, juzi wametupa pesa nusu na sisi tukachanganya zetu milioni mia moja tukawapelekea. Kwa hivyo tunalipa kwa mujibu wa utaratibu kama huu.

**Mhe. Hija Hassan Hija:** Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Fedha ya Biashara na Kilimo ambaye waziri anayejibu swali ndio waziri wangu na ni yeye mwenyewe Wizara yake ndio waliokuwa wakilalamika kuwa wana upungufu wa matrekta na wakatuahidi kwamba matrekta yanayokuja watayasambaza kwa wananchi Unguja na Pemba, na hawakutwambia kwamba matrekta yale watawapatia na Vikosi vya SMZ. Tukijua kwamba Vikosi vya SMZ mara kadhaa Waziri ametuahidi kwamba kuna fedha ambazo watatafuta matrekta kwa niaba ya vikosi vyao.

Ni kwa msingi gani sasa Mhe. Naibu Waziri atwambie ile hoja kwamba matrekta ya Wizara ya Kilimo ni machache leo akaona kuna haja ya kupeleka matrekta kwa vikosi huku wananchi wakilalamika Unguja na Pemba hawana trekta la kulimia. Hivyo hawakuona kwamba Wizara yake imekuwa wakitudanganya sisi.

**Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri sana yaliyojibiwa na Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili naomba kumjibu Mhe. Hija Hassan Hija swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza nataka niwaeleweshe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba Wizara ya Kilimo na Maliasili ni mali ya Serikali na Vikosi vilivyo chini ya Idara Maalum ni mali ya Serikali. Uwezeshaji wa Taasisi hizi zote unatokana na fedha inayotolewa na Serikali kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina. Na taasisi yoyote ile ambayo itataka kuchukua mkopo wowote inahitaji kupata dhamana ya Serikali. Kwa hiyo, hakuna ubaya kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa fedha zake wenyewe kuamua kwamba katika matrekta kumi ambayo Serikali imeyakopa, manane kubakia Wizara ya Kilimo na Maliasili na mawili kwenda katika Idara Maalum za SMZ.

Wizara ya Kilimo na Maliasili ndio yenye sera ya kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar wanalima vizuri na kuwa na uhakika wa chakula. Vikosi vya SMZ miongoni mwa jukumu ambalo wamepewa kikiwepo Kikosi cha Magereza, Chuo cha Mafunzo na Kikosi cha JKU ni moja kati ya Idara ambazo zinatekeleza sera za Wizara ya Kilimo na Mifugo chini ya Serikali.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe hizi fedha ni za Serikali, kwa hiyo Serikali inaweza ikaamua kupanga kulingana na mahitaji yalivyo. Kwa hiyo, Serikali imefanya jambo halali na halina matatizo yoyote, na hesabu hizo zote zitakwenda kama Naibu Waziri alivyosema. Ngapi zitatakiwa zitoke katika Mfuko wa Wizara ya Kilimo na ngapi zitatakiwa zitoke katika Kasma ya Idara Maalum. Hakuna tatizo na kwa sababu matrekta haya ni ya mkopo kama Wizara ya Kilimo itakuwa na uwezo zaidi wa kuongeza hayo matrekta mawili itakopa. Lakini kwa sasa kwa kuwa yalikuwepo matrekta kumi yaliyochukuliwa na dhamana na Serikali, Serikali ndio iliyoamua kwamba matrekta manane yabakie Wizara ya Kilimo na matrekta mawili yapelekwe Idara Maalum za SMZ kutekeleza sera ya kilimo. Ahsante sana.

**Nam. 78**

**Athari za Uchomaji Taka Karibu na Hospitali ya Mwembeladu**

**Mhe. Panya Ali Abdalla -** Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikifanya jitihada za makusudi ili kuwapatia wananchi wake huduma za afya. Na kwakuwa Hospitali ya Mwembeladu ni miongoni mwa vituo vilivyotengwa kwa ajili ya kutoa huduma ya uzazi salama kwa akina mama.

Na kwa kuwa kumekuwa na utaratibu uliozoeleka wa kuchoma taka za Hospitali karibu na maeneo ya Hospitali hiyo, ambapo moshi unaotokana na taka hizo huingia katika maeneo wanayolala wagonjwa wakiwemo kinamama na watoto wachanga.

(a) Je, kuendelea kuchoma taka hizo karibu na Hospitali hiyo hatuoni kuwa kunaweza kusababisha madhara kwa kinamama na watoto wanaozaliwa kwa kuvuta hewa ya moshi mchafu.

(b) Je, ni lini Serikail itajenga sehemu nyengine itakayotumika kuchomea taka hizo, ambayo itakukwa mbali na maeneo ya Hospitali hiyo, ili kuwanusuru kinamama na watoto kutokana na madhara ya kiafya yanayotokana na moshi huo.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya -** Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwanza naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tukiwa wazima wa afya leo na kuja kuwajibika katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Namba 78 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Mwakilishi kwa swali hili zuri sana, maana limeniwezesha na mimi kupata elimu ndani yake. Kwa hiyo, nimepata kuelimika, nimepata kutembelea maeneo husika, nimepata kuyaona hayo mashimo yenyewe ambayo nilikuwa siyajui kabla, nimepata kufika sehemu ambayo sijawahi kufika tokea nizaliwe, lakini swali hili limeweza kunisaidia kufika sehemu husika.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa uongozi wa Hospitali ya Mnazimmoja unajumuisha Hospitali mbili nyingine ambayo ni Hospitali ya Mwembeladu na Hospitali ya Kidongochekundu. Taka zinazozalishwa katika Hospitali ya Mwembeladu ni mazalia ya binadamu (kitaalamu *placenta*), pia taka nyingine huwa ni bomba za sindano na taka za mabaki ya chakula na mambo mengineyo yanayotokana na hospitali.

Kwa kuwa hospitali ya Mnazimmoja in mashine mbili za kuchomea taka. Moja, iliwahi kununuliwa kwa msaada wa fedha za msamaha wa madeni, kutokana na msamaha wa madeni ya Serikali na nyingine imepatikana kupitia Mradi wa *East Africa Public Health Laboratory* (*PHL*) *network* ambayo wanasaidia maabara ya Mnazimmoja kununua vitandanishi pia *regency* na baadhi ya mashine nyinginezo.

Taka zote za aina hiyo kutoka Hospitali ya Mwembeladu zinazohitaji kuchomwa zinaletwa Hospitali ya Mnazimmoja na huchomwa hapo.

Na kwa upande wa sindano na taka nyinginezo za aina hiyo basi Mhe. Mwenyekiti huletwa katika Hospitali ya Mnazimmoja ambapo kuna shimo maalum la kuzikia mazalia ya (*placenta pit*). Kwa hiyo, mazalia yote yanayotoka Hospitali ya Mwembeladu huzikwa katika shimo hilo kama mwongozo uliowekwa na Umoja wa Mataifa kupitia Shirika la Afya Dunia, kuna mwongozo maalum ambao umewekwa wa kuchota taka za hospitali, huwezi tu kuchoma hivi hivi kwa sababu zina madhara yake kimazingira na katika hewa. Na baadhi ya moshi unaotoka unaweza kugeuka yakawa maradhi mengine.

Kwa hiyo, kuna mwongozo maalum ambao umewekwa na Umoja wa Mataifa kupitia *WHO* wa udhibiti na utupaji taka ambao unajuulikana kama *WHO* (*Waste Management Disposal Rules and Regulation*).

a) Mhe. Mwenyekiti, kinachofanyika katika Hospitali ya Mwembeladu ni kuchoma taka za kawaida tu (*Domestic West*) ambazo madhara yake kiafya si makubwa kama vile ilivyokuwa kwa hizi taka nyingine nilizozitaja *Hospital West.* Lakini juu ya hilo namshukuru sana Mheshimiwa Mwakilishi kuleta swali hili tayari sasa hivi tumeshaandika barua kwa uongozi wa Hospitali ya Mnazimmoja ambapo, Hospitali ya Mwembeladu iko chini yake kuachana mara moja kuchoma taka ya aina yoyote ili kusiwe na moshi wowote ambao utamdhuru mama na mtoto.

b) Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la lini na wapi itajengwa sehemu nyingine ya kuchomea taka mbali na maeneo ya hospitali, suala hili linahitaji mashirikiano ya pamoja na mapana zaidi katika ya Taasisi mbali mbali za Serikali kama vile Idara ya Mazingira, Idara Mipango Miji, Baraza la Manispaa, Idara ya Mnazimmoja na Halmashauri za Wilaya mbali mbali ambazo maeneo yao yatapendekezwa kutumika kwa shughuli hiyo.

Taka za Hospitali naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mwakilishi si rahisi kuziteketeza pahala popote pale, huhitaji sehemu maalum na lazima iwe ni sehemu ambayo imetengwa kwa ajili ya shughuli hiyo ili isiweze kuleta madhara yoyote baadae yanayoweza kutokana na zile taka kubadilika katika mfumo aidha ikiwa shimo au kuchomwa isilete mabadiliko katika hali ya hewa. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwanza nataka nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo amesema suala hili limemfanya aweze kupata elimu kubwa kwa kufanya utafiti sehemu mbali mbali wa kwenda kuona jinsi gani hizi taka zinavyochomwa. Kwa kuwa amesema kama kwa sababu mimi nimeuliza suala hili kwa sababu nilikutia hicho kitendo kinafanyika, na ndio maana nikapata fursa ya kuuliza hili suala. Kwakuwa yeye mwenyewe amekiri kwamba madhara yapo, lakini si makubwa. Je, Mhe. Naibu Waziri utakubaliana na mimi kama bado ipo haja ya kufanya utafiti wa kina kuona taka hizi zinazochomwa katika mahospitali hazileti madhara kwa binadamu na tukielewa kwamba waliolazwa pale tayari ni wagonjwa tusije tukawaongezea magonjwa mengine.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, katika utafiti huu mdogo tuliofanya kuna aina tatu kama nilivyoeleza. Taka aina ya kwanza ni mazalia ya mwanadamu, yaani viungo au *placenta* au chochote kile kingine kinachotokana na mwili wa binadamu, taka aina ya kwanza.

Taka aina ya pili ni bomba za sindano pamoja na zile *chemical* zinazobakia, mfano vile vichupa vya dawa vidogo vidogo mnakuwa na *chemical* ambayo imebakia ndani.

Lakini taka aina ya tatu ni taka za kawaida, makaratasi yaliyokuwa yameshajazwa na kadhalika. Sasa hii taka aina ya tatu haileti dhara yoyote ila kwa moshi kama ulivyoeleza hapa katika swali lake la msingi, kwa moshi kumuathiri mama na mtoto katika wodi wanazolazwa hilo ni kweli, kwa sababu hata wewe zikichomwa karibu na nyumbani unakuwa huna raha ya kuvuta pumzi uzuri. Kwa hiyo, hilo limeshashughulikiwa tayari.

Lakini kwa utafiti wa hizi taka aina mbili lazima ipatikane sehemu maalum, mara nyingi huwa inatumika chombo kinachoitwa *incinerator* ambacho huchoma, moshi huwa mdogo unaotoka kwenye mazingira yetu na ule udhibiti wa ule moshi kutoa mdogo basi kuna kitu kama masinzi ambayo unatokana na ile *chemical* ambayo yale huchukuliwa nayo yakawa *dispose* baadae pia mabaki kama yale.

Kwa hiyo, taka hizi aina mbili bado tunaendelea nazo pale Mnazimmoja, ila katika swali la nyongeza ulivyouliza hospitali nyingine zinavyochoma hizi sasa tayari tumeshaandika barua na baada ya suala hili mimi nitahakikisha inaandikwa barua nyingine na Katibu Mkuu kwenda hospitali zote kama wana taka zozote za aina yoyote basi ziletwe sehemu husika za kuchomwa. Tatizo lilokuwepo mimi najua ni nini?

Moja ni uvviu mtu anaona uvivu kutoa taka sehemu iliyokuwepo. Aidha, mazalia ya binadamu anaona achimbe shimo pale pale atupe. Sasa hivi Mwenyezi Mungu atunusuru kuna maradhi kama haya ya *EBOLA* huwezi tu kuchimba pahala popote ukatupa mazalia ya binadamu, yanaweza kugeuka yale baada ya muda yakatokea mambo mengine Mwenyezi Mungu atunusuru *inshaallah*.

Lakini la pili ni usafiri, kwa sababu zile taka zinatakiwa kama zile bomba za sindano zina madebe maalum ambayo yanatupwa mule halafu baada ya pale hazikutani na mwanadamu tena mpaka zinapokwenda kutupwa. Sasa kuna usafiri wake maalum, lakini tutaendelea na jitihada kwamba wafuate hizi

sheria zilizowekwa na Umoja wa Mataifa kuzileta taka hizo aina mbili mazalia ya binadamu pamoja na taka hizo za *chemical*.

Kuhusiana na mambo ya makaratasi na fomu kuchoma sehemu ambayo iko mbali kidogo hiyo haina dhara. Ahsante sana.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Mhe. Mwenyekiti ahsante sana, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri yaliyoambatana na ufafanuzi mzuri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa hizi taka taka za hospitali ni *too much toxicative*, na kwa kuwa mimi nikiwa katika Kamati ile inayohusiana na mambo ya wanawake na ustawi wa jamii siku za nyuma nilikuwa napata muda sana wa kutembelea tembelea hazi hospitali zetu kubwa ikiwemo hii ya Hospitali yetu ya Mnazimmoja.

Na kwa kuwa kwa jicho langu nimewahi kuona taka sio kama ziko kwenye *incinerator* aah, zimewekwa katika ufukwe na tayari zinaanza kuchukuliwa na maji. Taka hizo nilipozichunguza kuna mabaki baki ya baadhi ya *chemical* pamoja na damu damu nyingi tu. Je, utaratibu ule wa Hospitali ya Mnazimmoja kuendelea ku-***cobute*** maji ya bahari umeshaondoka sasa au bado unaendelea, hilo la kwanza.

La pili, kwa kuwa wewe mwenyewe Mhe. Naibu Waziri umekiri kwamba bado pale Mwembeladu zinaendelea kuchomwa chomwa taka pale, na kwa kuwa hospitali ile ndio inatuzalishia nguvu kazi za keshokutwa maana yake ndio watoto wanazaliwa pale. Na kwa kuwa watoto wachanga uwezo wao wa kuingiza *oxygen* ni mdogo sana na huku pale taka zinachomwa huku zikiwa na baadhi ya hewa ukaa zinaingia hospitali na watoto wanapumua hewa ile. Je, huoni hizo taka ulizosema zinachomwa kidogo lakini kwa watoto wadogo moshi huo ni mkubwa na zitaathiri afya zao na hatimae kupunguza afya ya mtoto pamoja na mama yake.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, naomba tena nitoe ufafanuzi wa zile taka aina tatu ambazo Mhe. Saleh amezitaja pia taka zenye *toxication* ya hali ya juu ni kama yale mabomba ya sindano, zile *drip* zilizobakia pamoja na vile vichupa vidogo vidogo vyenye *chemical content* na *chemical* zinazohusiana na chemical. Na sio *toxication* tu pale pameshawahi pia kutoa kidogo mripuko kwa sababu ile *chemical reaction* ikitoka, *chemical reaction* nyingine zinasababisha mripuko. Kwa hiyo, imeshawahi kutokea kitu kuripuka na sauti kubwa tu ambayo imewahi kutokea pale Mnazimmoja.

Sasa mimi nadhani ningeomba siku moja tuandae ziara kwa ajili ya wale Waheshimiwa ambao watakuwa na *interest* ya kuona ile *incinerator* tuweze kwenda kuangalia. Kwa sababu ninavyoelewa mimi ila nitalifuatilia zaidi,

ninavyoelewa mimi sindano pamoja na masuala yote mengine hayaruhusiwi kabisa na kuna kampuni ambayo Dar Es Salaam *Bio-Chem* ambayo ina-*deal* na taka hizi wanakuja kuangalia wao ni kama *inspection agency* ya *UN* wanakuja kuangalia je, hizi taka zinadhibitiwa vipi.

Kuhusu kutupwa moja kwa moja pwani hilo, mimi sijaliona ila nachukua hii kama changamoto na nitafuatilia kuona kwamba maji yanakuwa *polluted* au vipi, kwa sababu hii ni hatari kubwa sana Mheshimiwa, hivyo ulivyoitamka peke yake ni hatari kubwa sana kwa sababu hata sekta ya utalii ikijua jambo hilo, basi ni hatari kwa Zanzibar na uchumi wake pia. Kwa sababu linaweza kuathiri utalii. Hilo mimi sikuliona na halipo kwa muda huu ila tutalifuatilia kuchunguza kama je, kweli hivyo vitu vinafanyika kutupwa baharini.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nikiendelea na sehemu (b) ya swali sijalipata vizuri swali la pili naomba alirudie kidogo.

**Mhe. Saleh Nassor Juma:** Kwa kuwa Mheshimiwa nilikuwa nazungumzia Hospitali ya Mwembeladu ndio *in machine* inayotufyatulia vifaranga vyetu pale nakusudia ndio inayozalisha na wewe mwenyewe umekiri kwamba pale panaendelea kuchomwa taka taka, lakini ndio ujue kama zinaendelea wakati zinachomwa zina-*pollute air* na pale pana watoto wachanga, na bahati mbaya sana pale kuna wale *kangaroos* wale watoto amabo hata hawajatimiza siku zao za kuzaliwa wapo pale Mwembeladu, wamewekwa na mama zao. Sasa kuendelea watoto wachanga namna ile kuwachomea taka na moshi ukiingia hospitali je, utaratibu ule si kuathiri zile afya za wale watoto.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana ni kweli kama nilivyojibu pale awali kwamba taka taka hizi hazitakiwi kuchomwa na kupitia Baraza hili leo tunawaambia waache mara moja kuchoma taka hizo na barua pia itafuata nyengine. Kupitia Baraza hili waache kuchoma taka hizo mara moja, taka zote ziletwe sehemu husika ambazo wao wanazijua wameshaelimishwa na wameshafunzwa, na barua rasmi itafuatilia ambayo na nakala yake pia nitaiwasilisha hapa Barazani. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

**Mhe. Ali Salum Ali:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza suala dogo la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, wakati Mhe. Naibu Waziri anajibu masuala yake ametamka kwamba wameshatoa maagizo kwenye vituo kwa kukataza kuchoma taka kwa zile taka ambazo ni hatarishi kwa maisha ya mwanadamu, na akaendelea kusisitiza kwamba atamtaka Katibu wake Mkuu aendelee kuandika barua ya maagizo ya kutaka wahusika wa vituo vyote waache kuchoma taka hatarishi, suala langu liko hapa Mheshimiwa Mwenyekiti.

Kwa kuwa Wizara ya Afya inapiga kelele katika suala zima la kutokuwa na mafuta ya kutosha katika kutoa huduma kwa vituo vyake. Je, haoni agizo analolitoa kwa vituo vya afya itakuwa ni agizo ambalo halitekelezeki na kuwatia hatiani wafanyakazi pasipo na hatiya.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Kuna utaratibu maalum ambao utapangwa na Wizara kwa kuwasilisha taka hizo, kuna utaratibu maalum utapangwa na tayari umeshapangwa wa kuzikusanya taka kama hizo na asiwe na hofu kwa suala la mafuta kwa hizi hospitali tatu ambazo zimo chini ya uongozi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, basi tatizo hilo litawezekana kudhibitiwa. Asiwe na wasi wasi juu ya bajeti ya mafuta, pia tuna miradi mbali mbali pale Wizarani ambayo tutaweza kukidhi haja kwa matumizi kama hayo. Ahsante sana.

**Nam. 79**

**Ajira kwa Walinzi**

**Mhe. Panya Ali Abdalla** - Aliuliza:-

Kwa kuwa Wizara ya Afya inatumia wafanyakazi wanaotumika kulinda maeneo mbali mbali ya Wizara ili kuweka ulinzi na usalama wa watu na mali zilizomo katika maeneo hayo.

(a) Je, wafanyakazi hao wameajiriwa kisheria kwa kusaini mikataba ya ajira.

(b) Ikiwa hawajapata ajira rasmi kwa mujibu wa sheria; Je, utaratibu gani utatumika kuwapatia haki zao, wakati muda wao wa kustaafu utakapofika.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya** - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Bi Panya Ali Abdalla swali lake Nambari 79 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya inatumia wafanyakazi wake walinzi kwa kulinda maeneo mbali mbali ya wizara ikiwemo na Hospitali ya Mnazi Mmoja pamoja na hospitali nyengine zote na Vituo vya Afya, ili kuweka

usalama katika maeneo hayo ambayo ni muhimu kwa binadamu na zile dawa ambazo zinawekwa katika maeneo hayo.

Wizara inawapata wafanyakazi hao (walinzi) kwa njia mbili kuu. Kwanza, kuwaajiri moja kwa moja kisheria na kusaini nao mikataba ya ajira ambapo haki na maslahi yao yanapatikana kama utaratibu wa kanuni za utumishi zinavyoelekeza serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, njia kuu ya pili, wizara kujaza mikataba na makampuni binafsi yanayoshughulika na ulinzi baada ya kupitia taratibu zote za ushindani. Wizara inatia mikataba hiyo saini na inawalipa fedha kwa makampuni moja kwa moja na kampuni hizo zinatupatia walinzi ambao maslahi na stahiki zao zinalipwa na wamiliki wenyewe wa kampuni hizo. Njia hii inatumika zaidi kwa hivi sasa katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja. Ukifika pale wale wanaovaa nguo nyekundu ndiyo wa kampuni hiyo.

**Mhe. Panya Ali Abdalla:** Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri malalamiko haya yanatokana na wafanyakazi wenyewe ambao ndio wanaolalamika.

Je, Mhe. Naibu Waziri uko tayari kuwasikiliza wafanyakazi hawa ili kero yao hii ya uajiri iweze kujua tatizo limesababishwa na nini.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, namjibu Mheshimiwa Mjumbe kuwa niko tayari na ninawakaribisha ofisi kwangu, sijawahi kusikia kero hiyo waje nayo hiyo kero na ninaamini tutaweza kuitatua kwa kukaa pamoja na kujadiliana pamoja na uongozi wa wizara. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kuweza kunipa ruhusa ya kuweza kumuuliza Naibu Waziri swali la nyongeza ambalo lina sehemu mbili. Kwanza nimpe hongera sana Mhe. Naibu Waziri na laiti angekuwa amesomea fani hiyo basi angekuwa ame-*qualified* vizuri sana. Hiyo nampongeza kwa majibu yake matamu sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, swali langu liko hapa. Kabla hamjaanza kutafuta makampuni ilikuwa vijana wanavaa nguo rangi ya kijani na walikuwa wanafanya kazi vizuri sana. Je, vijana wale hivi sasa wako wapi? Na kama ni hivyo, kwa nini sasa hivi usifanye kazi ya ziada kwa ushupavu wako wewe ninavyokuamini ukaweza kuwatafuta na ukajua haki zao ziko wapi.

Lakini pili, tuna vituo vyetu ambavyo kwenye mashamba huko navyo vina vitu vya thamani. Kwa nini Mheshimiwa kwa kuwa kule kampuni hazijafika na kama hazijafika kwa nini usiendeleze kufikisha Kampuni zile ili kuendeleza ulinzi pasipokuwa kutafuta watu wengine.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba tupokee pongezi, namshukuru sana na mimi jambo nililokuwa silijui sioni tabu wala sioni haya kusema silijui nitalisema hapa hapa Barazani. Hawa askari wa Kijani siwajui waliokuwepo wala sijawahi kuwaona, ila nitakachokifanya nitafuatilia kuweza kujua na nitamuomba Mheshimiwa Makame Mshimba Mbarouk aje pale ofisini kwetu tuzungumze, anifahamishe mana Mwenyezi Mungu amenijaalia bahati nimekwenda mara chache sana hospitali. Kwa hiyo, hata hao askari wa kijani sijawahi kuwaona hapo kabla. Kwa hiyo, angalau tupate kuwajua hawa askari wa kijani anaozungumzia yeye ni wepi waliokuwepo tuweze kuweka mambo sawa.

Kuhusu vituo vyengine vya afya vilioko katika majimbo mbali mbali au mashamba, suala hili nilifuatilia wakati natafuta jibu la msingi hapa na nikagundua kwamba mara nyingi wale walinzi walioko katika vile vituo vya mbali na mjini au vilioko mashamba huwa wanaingia katika masuala ya jamii pamoja, yaani uongozi wa kituo pale. Uongozi wa jamii huwa wanachangishana fedha kupitia fedha zinazochangiwa na wagonjwa mbali mbali kupata huduma na fedha zile zinatumika kuwalipa mishahara walinzi wale. Huo ni utaratibu ambao Wizara ya Afya nimeukuta mimi wamekubaliana pamoja na jamii husika ama shehia husika katika maeneo hayo. Ni utaratibu ambao unaendelea vizuri haujaleta madhara yoyote mpaka sasa hivi. Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti.

## UTARATIBU

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Sikukusudia kusema wale walikuwa ni askari wa kijani hapo mwanzo, walikuwa wanavaa shati za kijani tu hao vijana wenyewe, ndiyo lengo langu nililokusudia naomba kusahihisha katika *hansard*.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante umeeleweka.

**Mhe. Naibu Waziri wa Afya:** Mhe. Mwenyekiti, kwa utaratibu huo naomba kumuuliza hivi sasa wanavaa rangi gani? Kwa sababu anasema mwanzo walikuwa wanavaa kirani sasa hivi wanavaa rangi ipi?

**Mhe. Mwenyekiti:** Basi mtazidi kuelewana mtakapokuwa mko pamoja.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Wamechukuliwa na wizara yako hapo mwanzo kabla ya kampuni kufanya mkataba, sasa wale mpaka leo hawajajijua wako wapi ni kwamba wapo tu, wengine wapo nje. Wengine wamo mle mle, lakini mle mle wako katika mikono ya wizara hawako katika mikono ya kampuni kwa sababu wa kampuni wanavaa rangi ya buluu na nyeusi.

**Mhe. Mwenyekiti:** Mhe. Naibu Waziri na Mhe. Mjumbe mtakaa pamoja mtaweza kuya-*sort-out* haya baadae ahsante. Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Mswada wa Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar ya Mwaka 2014

*(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kusoma kwa mara ya kwanza Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Baraza la Manispaa Nam. 3 ya mwaka 1995 na Sheria za Halmashauri za Wilaya na Mabaraza ya Miji Nam. 4 ya mwaka 1995 na kuanzisha upya Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar ya Mwaka 2014, kwa madhumuni ya kuanzisha Serikali za Mitaa uwezo wake, kazi na wajibu, muundo, mpangilio, fedha na mambo mengine yanayohusiana na hayo naomba kusoma kwa mara ya kwanza.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante, Katibu.

### Mswada wa Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar ya Mwaka 2014

*(Kusomwa kwa mara ya Pili)*

**Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:** Mhe. Mwenyekiti, Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Baraza la Manispaa Nam. 3 ya mwaka 1995 na Sheria za Halmashauri za Wilaya na Mabaraza ya Miji Nam. 4 ya mwaka 1995 na kuanzisha upya Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Zanzibar ya Mwaka 2014, kwa madhumuni ya kuanzisha Serikali za Mitaa, uwezo wake, kazi na wajibu, muundo, mpangilio, fedha na mambo mengine yanayohusiana na hayo naomba kusoma kwa mara ya pili.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Muhtasari ya Mswada wa Sheria ya Serikali za Mitaa Zanzibar.

## Utangulizi

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia kuwa na afya njema na hali ya uzima ambayo imetuwezesha kukutana tena leo hii katika mkutano huu.

Mhe. Mwenyekiti, aidha nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali kunipa fursa ya kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Serikali za Mitaa Zanzibar katika Baraza lako tukufu. Shukurani za pekee zimuendee Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dr. Ali Mohammed Shein kwa kuniagiza kuwasilisha rasmi Mswada wa Sheria ya Serikali za Mitaa katika Baraza lako tukufu jambo ambalo linanizidishia ari, nguvu na kazi ya kufanya kazi kwa kuzingatia misingi ya utawala bora kutokana na maelekezo yake anayonipa mara kwa mara. Aidha, namshukuru kwa kuona umuhimu wa kupatikana kwa sheria hii na kuagiza kuleta katika kikao hiki kitukufu kwa hati ya dharura.

Mhe. Mwenyekiti, hii inaonyesha jinsi anavyojali maendeleo ya wananchi na kuwapa fursa kufanya maamuzi ya msingi yanayohusu maendeleo yao, ambalo ndilo lengo kuu la mswada huu na Sera za Serikali za Mitaa ambao alisimamia kwa nguvu zake zote na kuhakikisha kuwa inakamilika kwa wakati na ndio msingi wa mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, nalishukuru Baraza la Mapinduzi kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kujadili na kupitisha mswada huu, maelekezo na miongozo yao yaliweza kufanikisha kukamilika kwa mswada huu na kuruhusu kuwasilishwa katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu umejadiliwa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Ussi Jecha Simai, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Chaani. Aidha, nawashukuru Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi ambao walishiriki pamoja na Kamati kuujadili mswada huu na kuufanyia marekebisho maeneo ambayo yalikuwa na mapungufu na kwa sasa uko katika hali nzuri. Nawashukuru sana kwa kazi kubwa waliyoifanya uzoefu, uelewa na umahiri wao ndio uliofanikisha kuwasilisha mswada huu katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, pia nachukua fursa hii kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Mhe. Said Hassan Said, kwanza kwa kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tunampongeza sana.

Pili, kwa umahiri wake mkubwa aliyoonyesha katika kusimamia ukamilishaji wa Miswada yetu ambayo alikuwa na muda mfupi wa kuishughulikia, lakini ameweza kuifanya kazi hiyo bila ya kujali muda wa kuweza kuikamilisha na kuniwezesha leo kuwasilisha moja ya miswada hiyo ambao ni Mswada wa Sheria ya Serikali za Mitaa.

Aidha, nawashukuru watendaji wa ofisi yake ambao walifanya kazi usiku na mchana bila ya kuchoka kwa kuifanyia marekebisho mbali mbali ya kitaalamu ambayo yalikuwa ni muhimu kufanyika kabla ya kupelekwa Idara ya Uchapaji.

Vile vile, napenda kutoa shukurani na pongezi kwa Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa utekelezaji wa majukumu yake katika kuhakikisha kuwa gurudumu la maendeleo linasonga mbele hususan kwa ofisi hii ambayo ni takriban ya mwaka mmoja na miezi miwili sasa toka kuundwa kwake upya. Nami nikiwa waziri mwenye dhamana ya kusimamia ofisi hii, bila ya kuwasahau watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, kwani ushirikiano wao kwangu ndio chanzo cha mafanikio haya.

Pia naomba niwashukuru wafanyakazi wa Idara ya Upigaji Chapa iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuweza kukamilisha kazi ya upigaji chapa ya mswada huu. Nawashukuru sana.

**Chimbuko la Mswada**

Mhe. Mwenyekiti, chimbuko la mswada huu ni hali ya kuweka mfumo wa kugatua madaraka au kupeleka nguvu zaidi za maamuzi kutoka Serikali Kuu hadi ngazi za Serikali za Mitaa kisheria. Kwa muda mrefu upelekaji wa madaraka kwa wananchi imekuwa njia kuu ya kukuza demokrasia ni agenda ambayo utekelezaji wake haukufanikiwa sana. Baada ya mageuzi mbali mbali yaliyofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ukiwemo MKUZA, kulipelekea kuandaliwa sera mpya ya Serikali za Mitaa ambayo utekelezaji wake unahitaji nguvu za kisheria, ili kukabiliana na changamoto zilizosababisha kutofanikiwa sana katika jitihada zilizofanyika siku za nyuma.

**Lengo na Madhumuni ya Mswada**

Mhe. Mwenyekiti, Mswada wa Sheria ya Serikali za Mitaa una lengo na madhumuni ya kusimamia utekelezaji wa kazi za Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kuwashirikisha wananchi wa ngazi za chini katika kufanya maamuzi ya kimaendeleo.

**Maelezo ya Mswada**

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu umezingatia mahitaji ya Serikali za Mitaa kwa matakwa ya sasa na baadae, ambayo yametokana na maoni na michango ya wahusika mbali mbali wakiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ambayo yamezingatiwa katika mswada huu.

**Muundo wa Sheria**

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kuwasilisha Muhtasari wa Mswada wa Sheria ya Serikali za Mitaa Zanzibar ambao umegawika katika Sehemu Tisa kama ifuatavyo:

**Sehemu ya Kwanza**

Sehemu hii ina vifungu viwili ambavyo ni jina fupi la sheria na tarehe ya kuanza kutumika pamoja na tafsiri ya maeneo.

**Sehemu ya Pili**

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii ina vifungu kumi ambavyo ni kifungu cha tatu hadi kumi na mbili vinavyoelekeza Mamlaka ya Serikali za Mitaa, eneo la Mamlaka ya Serikali za Mitaa, vyanzo vya sheria vya Serikali za Mitaa, lengo la Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Misingi ya Utawala, mgawanyo wa Serikali za Mitaa, aina ya Mabaraza ya Serikali za Mitaa na Ugatuzi wa Madaraka.

**Sehemu ya Tatu**

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii ina jumla ya vifungu vitano kuanzia kifungu cha 13 hadi 17, ambavyo vinaelekeza kuanzishwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, sifa za kuanzisha Serikali za Mitaa, taratibu za kuanzisha Mamlaka za Serikaliza Mitaa na Hati ya uanzishwaji wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

**Sehemu ya Nne**

Mhe. Mwenyekiti, sehemu hii ina vifungu 34 kuanzia kifungu cha 18 hadi 51 ambavyo vinaelezea muundo, kazi na uwezo wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kuanzishwa kwa Mamlaka ya Jiji, Baraza la Manispaa, Baraza la Mji, Halmashauri za Wilaya na Mabaraza ya Wadi na Shehia, kazi na Mamlaka ya Jiji, Baraza la Manispaa, Baraza la Mji na Halmashauri za Wilaya. Muundo wa Mamlaka ya Jiji, Baraza la Manispaa, Baraza la Mji na Halmashauri za Wilaya.

Viapo vya Madiwani, muda wa kuwepo madarakani Meya, Naibu Meya, Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Marupurupu na maposho ya Meya, utaratibu wa kuondoshwa Meya na Mwenyekiti, uteuzi, kazi, wajibu na nafasi za Mkurugenzi. Sifa na kazi za kuanzishwa kwa Kamati ya ushauri wa Wadi na Shehia na Karani wa Baraza la Wadi.

**Sehemu ya Tano**

Mhe. Mwenyekiti, sehemi hii ina vifungu tisa kuanzia kifungu cha 52 hadi 60 ambavyo vinaelezea kamati na idara za mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kuanzishwa kwa Kamati za Maendeleo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kazi za Kamati za Maendeleo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Kamati za Kudumu za Mamlaka ya Jiji, Manispaa, Baraza la Mji na Halmashauri ya Wilaya, Kati na uwezo wa Kamati za Kudumu, mipango ya maendeleo ya Serikali za Mitaa, Idara za Mamlaka za Serikali za Mitaa, kazi za Idara, Wajibu wa Mkuu wa Idara na Mikutano na taratibu za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, Sehemu ya Sita, sehemu hii ina vifungu vinne kuanzia kifungu cha 61 hadi 64 ambavyo vinaelezea wafanyakazi wa mamlaka ya Serikali za Mitaa wafanyakazi wa muda, uwezo wa kazi na uwawajibikaji wa maofisa.

Mhe. Mwenyekiti, Sehemu ya Saba, sehemu hii ina vifungu 16 kuanzia kifungu cha 65 hadi 80 ambavyo kwa ujumla wake vinaelezea kuhusu Mipango, Fedha, Uchumi na Maendeleo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kazi na wajibu wa vitengo mbali mbali ikiwa ni pamoja na Kitengo cha Mipango, Ukaguzi, Uhasibu, Uchumi na Maendeleo, Utelekezaji na Usimamizi wa Mipango ya Baraza, Vyanzo vya Fedha za Serikali za Mitaa, Vianzo vya Mapato ya Serikali za Mitaa, Michango ya Jamii, Misaada na Mikopo kuanzishwa kwa Mfuko wa Serikali za Mitaa na masuala ya Bajeti kwa Ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, Sehemu ya Nane, sehemu hii ina vifungu vitano kuanzia kifungu cha 81 hadi 85, vifungu hivi vinaelezea taratibu za kisheria, makosa na adhabu.

Mhe. Mwenyekiti, Sehemu ya Tisa, sehemu hii ina vifungu 11 kuanzia kifungu cha 86 hadi 95 ambavyo vinaelekeza juu ya mambo ya ujumla ya sheria ikiwemo Mikutano ya Wazi, Ukomo, Uwajibikaji Kisheria, Uwezo wa Kuvunja Baraza kabla ya kumaliza muda wake, Polisi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Mawasiliano baina ya Taasisi za Serikali na Mabaraza,

Michango ya Mabaraza, Muda wa mpito, Utungaji wa Kanuni, Kufutwa kwa Sheria zinazotumika sasa.

**Hitimisho:**

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha kwenye Baraza lako Tukufu mswada huu kwa kufuata taratibu za kisheria na Kanuni za Baraza la Wawakilishi ili muupitie, muujadili, mtoe ushauri wenu na hatimae muidhinishe mswada huu na kuwa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante, hoja imekubaliwa Mwenyekiti wa Kamati.

**Mhe. Ussi Jecha Simai (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala):** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ya kusoma maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Baraza la Manispaa namba 3 ya mwaka 1995 na Sheria za Halmashauri za Wilaya na Mabaraza ya Miji namba 4 ya mwaka 1995 na kuanzisha upya Sheria ya Mamlaka ya Serikili za Mitaa Zanzibar ya mwaka 2014 kwa madhumuni ya kuanzisha Serikali za Mitaa uwezo wake, Kazi, Wajibu, Muundo, Mpangilio, Fedha na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, nitangulize shukurani zangu za dhati kwa Muumba wa Mbingu na Ardhi, uhai na umauti na kila kilichopo, kinachoishi na kuvuta pumzi, naye ni Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa neema kubwa aliyotupa ya uzima na uhai wa afya tele ambao ametubarikia sisi waja wake tuliokusanyika hapa bila ya gharama yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru na wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kusimama mbele ya chombo hiki cha uwakilishi wa wananchi kwa kusoma maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi ambayo ndiyo ngome ya matumaini na tegemeo la kujadili mambo yanayohusu ustawi na mustakbali wao katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, muda mrefu umepita baada ya Mkutano wa Bajeti, ambapo mambo mengi yamebadilika tokea wakati huo yakiwemo mabadiliko na teuzi za watendaji wakuu mbali mbali katika Wizara na Taasisi ambazo Kamati hii inazisimamia.

Aidha, nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutekeleza vyema matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka

1984, katika vifungu vya 43 (2), 53 na 55 kwa kufanya uteuzi katika nyadhifa mbali mbali katika wizara, Idara na taasisi mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukuwe nafasi hii kupongeza uteuzi wa mawaziri na manaibu waziri wakiwemo Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya, ambaye ameteuliwa kuwa Waziri wa Kilimo na Maliasili, Mhe. Juma Duni Haji kuwa Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano na Mhe. Rashid Seif Suleiman, kuwa Waziri wa Afya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa fahari kubwa nipongeze Uteuzi wa Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, kuwa Naibu Waziri wa Afya ambaye alikuwa Mjumbe mahiri wa Kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, nisisahau pia kutumia muda huu mchache kupongeza wateule wengine katika ngazi za mikoa, wilaya na zaidi Uteuzi wa mwanasheria mkuu mpya ambaye ni Mhe. Said Hassan Said, napenda kusema kuwa kwa namna yoyote teuzi hizi zilivyofanyika na kwa mazingira yoyote zilivyotokezea ni kheri na tumshukuru Mungu kwa kila linalojiri katika maendeleo ya nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, wakati naelekea kusema machache kati ya mengi ambayo ningependa kusema kuhusu maoni ya Kamati katika mswada huu, naomba pia kutumia sekunde chache sana kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ambao kwa niaba yao, nimesimama hapa kuwasilisha maoni ya Kamati, kwa kazi kubwa na ngumu waliyofanya ya kuuchunguza mswada huu tokea asubuhi ya siku ya tarehe 27/10/2014 hadi saa nne za usiku wa siku hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa jitihada zao hizo, naomba nichukuwe nafasi hii nitambuwe mchango mkubwa walioutoa wakati wa kupitia mswada huu kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Ussi Jecha Simai | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Abdalla Juma Abdalla | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Wanu Hafidh Ameir | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Nassor Salim Ali | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Bikame Yussuf Hamad | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Suleiman Hemed Khamis | Mjumbe |

Mhe. Mwenyekiti, wakati wa kupita mswada huu, Kamati yetu ilisaidiwa na makatibu wawili kutoka Afisi ya Baraza la Wawakilishi ambao ni:

1. Ndg. Khamis Hamad Haji; na
2. Ndg. Salum Khamis Rashid.

Bila kuwasahau Katibu wa Baraza la Wawakilishi na Mshauri Mkuu wa Sheria wa Baraza pamoja na wanasheria na watendaji mbali mbali wa Afisi ya Baraza ambao Kamati inatambua na Kuthamini mchango wao walioutoa wakati wa kupitia mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, msema kweli ni mpenzi wa Mungu, naomba nikiri kuwa kazi ya kuupitia mswada huu kwa kipindi kifupi tu kilicholetwa ingelikuwa ngumu sana, kwani itakumbukwa kuwa mswada huu umeletwa kwa hati ya dharura na Kamati imepatiwa siku moja na siku hiyo hiyo kutakiwa kuujadili.

Hivyo, naomba nitoe shukurani za pekee na za dhati kabisa kwa uwakilishi wa Wajumbe wa Kamati ya Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza wakiongozwa na Mwenyekiti wao, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi mahiri na makini wa Jimbo la Kwamtipura ambao walitoa mchango mkubwa kwenye Kamati yangu wakati wa kupitia mswada huu na kuifanya kazi hii ya ghafla na dharura kuwa ya ufanisi, naomba niwatambue Wajumbe waliowakilisha Kamati ya Wenyeviti wakati wa kupitia mswada huu kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Hamza Hassan Juma | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Salmin Awadh Salmin | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Mahmoud Muhamed Mussa | Mjumbe |

Mhe. Mwenyekiti, nimechukuwa muda wako mrefu kidogo kutoa pongezi hizo si kwa nia ya kupoteza muda bali ni kutokana na umuhimu wa michango na mawazo mengi ya watu mbali mbali niliotangulia kuwataja, ambao maoni na michango yao imewezesha leo hii kuwasilishwa kwa Mswada wa Kuanzisha upya Sheria ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2014, kujadiliwa mbele ya Baraza hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Masharti ya Kanuni ya 84. fasili ya (7) na kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, naomba nianze kuwasilisha maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi ambayo imeshirikiana na wizara kuchunguza mswada huu uliowasilishwa na Mhe. waziri, muda mchache uliopita.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu umewasilishwa hapa kwa hati ya dharura kwa mujibu wa Kanuni ya 80 na 83 (3) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la

Wawakilishi, toleo la mwaka 2012 na kuwasilishwa kwenye Kamati yetu kwa ajili ya kuuchunguza kwa mujibu wa Kanuni ya 83 (4) ya Kanuni hizo, Kamati yangu inakubaliana na sababu ilizoelezwa na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa na Idara Maalumu, kuhusu uharaka wa kuletwa mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nieleze mbele ya Baraza lako kuwa Kamati yangu ilipokuwa inazitembelea Afisi za Serikali za Mitaa, zikiwamo Halmashauri na Mabaraza ya Miji na Manispaa, imegunduwa changamoto nyingi za utekelezaji wa shughuli zao kutokana na mapungufu mbali mbali ambayo asilimia kubwa yametokana na mapungufu ya sheria zilizopo ambazo zinakwaza utekelezaji wa ufanisi wa shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, imekuwa ni kilio cha Serikali za Mitaa tulizozitembelea kuomba mswada huu uletwe haraka hapa Barazani kwa ajili ya kupitishwa kuwa sheria ili changamoto hizo zinazokabili utelezaji wa majukumu yao ziweze kutatuliwa kwa sheria mpya.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na sababu zilizoelezwa na Mhe. waziri, wakati akiwasilisha mswada huu kwa hati ya dharura muda mchache uliopita, Kamati yangu imeshuhudia jinsi sheria zilizopo zinavyokwamisha jitihada za Serikali za Mitaa za kuweza kukabiliana na changamoto za kimaendeleo katika maeneo yao kama vile kupata wataalamu, kumudu na kudhibiti vyanzo vya mapato, kusimamia utekelezaji wa kazi, uwezo na wajibu wao kwa sheria madhubuti. Hivyo basi, mswada huu umeletwa katika kipindi ambacho kuchelewa kwake kunaendeleza changamoto hizo na nyengine nyingi katika Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka tutambuwe mfumo wa uendeshaji wa Serikali kuhodhi kila shughuli hata ya kuzoa taka, kwa mfano kuwa umepitwa na wakati, Serikali nyingi za kileo zimekuwa zikijikita katika mambo makuu ya kisera na kuziwacha kwa kuziwezesha Serikali za Mitaa kufanyakazi za kimaendeleo kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza hili limewahi kupitisha sheria nyingi ambazo baadhi yake utekelezaji wake unakuwa siyo wa ufanisi kutokana na kutokuwapo kwa sheria madhubuti ya Serikali za Mitaa, mfano wa sheria hizo ni Sheria ya Amri ya Barabara, Sura ya 134 ambayo baadhi ya mgawanyo wa majukumu yake ya kushughulikia barabara za ndani unaelekezwa kwa Serikali za Mitaa. Kwa sababu hiyo basi, endapo Serikali hizi hazitawekewa sheria madhubuti ya kufanyakazi zao basi utekelezaji wa kazi hizo na shughuli nyengine utakuwa mgumu.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeuchunguza mswada huu kwa kushirikiana na wizara, wataalamu kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu na kushauri marekebisho mbali mbali ya mswada huo kwa kufuta baadhi ya vifungu, kurekebisha, kuandika upya, kuhamisha baadhi ya vifungu kutoka sehemu moja na kuviweka sehemu nyengine pamoja na kurekebisha makosa kadhaa ya kiuandishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 83(7), Kamati yetu haikupewa mamlaka ya kufanya mabadiliko katika mswada huu, isipokuwa kumshauri Mhe. waziri, kufanya mabadiliko katika mswada huo, Hivyo, kamati yangu imewasilisha nakala za mapendekezo ya marekebisho ya mswada katika maeneo mbali mbali kama nilivyotangulia kusema hapo awali. Nakala hizo zimeshawasilishwa kwa Wajumbe kwa ajili kuwasaidia kutoa maoni na michango yao na kumshauri zaidi Mhe. waziri, ili mswada huo upitishwe na Baraza hili na baadae iwe sheria inayopendekezwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Wajumbe wa Baraza hili kuchangia kwa umakini mswada huo muhimu katika maendeleo ya nchi yetu na hatimaye kuupitisha na kuwa sheria ili kuziwezesha Serikali zetu za Mitaa kufanyakazi zao kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba nimshukuru kwa dhati na hiari ya moyo wangu Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa mashirikiano yake makubwa pamoja na watendaji wake waliotupatia kuanzia mwanzo kuanza kujadili mswada huu hadi leo hii kuletwa katika Baraza lako Tukufu.

Lakini pia, nimpongeze kwa ujasiri mkubwa ambao mswada huu umepitia katika awamu nyingi kuna zaidi ya mawaziri wanne naweza kusema mawaziri watano waliokuwa wakiongoza wizara hii, mswada huu haukuthubutu kupita katika Baraza hili. Kwa hiyo, nimpongeze kwa ujasiri wake na kwa nia yake njema.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nachukuwa nafasi hii kukushukuru tena kwa kunivumilia kwa muda huu mchache sana kuwasilisha maoni ya Kamati yangu mbele ya Baraza lako tukufu. Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Nakushukuru sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk.

**Mhe. Makame Mshimba Mbarouk:** Mhe. Mwenyekiti, kwa kutumia haki ya Kanuni na kwa kuwa mswada huu ni mkubwa sana na ni mzito kifungu cha 64, ukurasa wa 48 na ni muda wenyewe ni fupi tuliopewa mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu unaelekea kwa wananchi na sio tu kukaa tukasema kuwa leo hii hii tuuchangie haitokuwa sahihi. Kwa hiyo, kifungu hiki cha 64, naomba tuakhirishe Baraza lako Tukufu tupewe muda kesho ili tuje tuweze kuuchangia kwa fasaha kabisa ili kutoa ridhaa kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja na Wajumbe wote wasimame waniunge mkono.(*Makofi*)

**Mhe. Mwenyekiti:** Ahsante sana Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, kwa kuwa makini sana na kuamua kutaka kufanya vitu ambavyo vile wananchi walikuwa wamekuagizeni kuja kufanya katika Baraza letu hili tukufu.

Waheshimiwa Wajumbe, ni kweli mswada huu ni mzito sana na ni mkubwa na jana umemalizika wakati dhiki kidogo. Sasa kabla sijawahoji Waheshimiwa Wajumbe, kutokana na hoja hii ambayo Mhe. Makame Mshimba, ameitoa sasa niseme tu kwamba ni kweli tunakubali muda ni mdogo sana na panahitajika kupata muda kwenda kuupitia, narejea tena kwenda kuupitia mswada huu na baadae muje kuuchangia.

Sasa kabla sijampisha mwanasheria mkuu labda tufanye utaratibu niwahoji Wajumbe, wanaokubaliana kwamba tuakhirishe Baraza letu hadi kesho asubuhi saa 3:00, wanyooshe mkono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

Sasa kwa mujibu wa taratibu za kibaraza au kibunge tumuombe mwanasheria m.kuu kwa kutumia kifungu cha 23, nafikiria tumsikilize ili tuweze kufanya utaratibu wa kisheria. Mhe. mwanasheria mkuu.

**Mhe. Mwanasheria Mkuu:** Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu kwa kutumia Kanuni ya 23, fasili ndogo ya pili, niakhirishe mjadala wa leo kama ambavyo imetolewa hoja na Mhe. Mwakilishi, mpaka hapo kesho saa tatu asubuhi. Naomba kutoa hoja.

**Mhe. Mwenyekiti:** Sawa hoja imeungwa mkono na Wajumbe wote wanaokubaliana na hoja wanyooshe mkono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa kabla hatujaakhirisha kikao chetu hichi kuna tangazo hapa. Wale Wajumbe wa Kamati ya Uongozi tunaombwa baada ya kwisha kuakhirisha kikao hichi tupande juu katika ukumbi wetu wa kawaida

kuendelea na kikao chetu. Baada ya maelezo hayo, sasa niseme tu kwamba naakhirisha kikao hiki hadi kesho asubuhi saa 3:00 barabara bila ya kukosa Wajumbe wote muwepo, naomba kuakhirisha.

*(Saa 4:40 asubuhi Kikao Kiliakhirishwa hadi tarehe 29/10/2014 saa 3:00 asubuhi)*